**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

# TAARIFA YA HALI HALISI YA MAENEO YA WAZI NA BURUDANI NCHINI

***(KATIKA KIKAO KAZI CHA KUSITISHA UTARATIBU WA KUPANGISHA NA KUTUMIA MAENEO YA WAZI KWA MATUMIZI MENGINE)***





**Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,**

**Mtaa wa Ardhi,**

**S.L.P 2908,**

**40477DODOMA.**

## YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ..... 3

2.0 MATUMIZI YA MAENEO YA WAZI ..... 4

3.0 MADHARA YA KUKOSEKANA KWA MAENEO YA WAZI ..... 5

4.0 USIMAMIZI NA UDHIBITI WA MAENEO YA WAZI ..... 6

5.0 UTARATIBU WA KUPANGISHA MAENEO YA WAZI ..... 7

6.0 HALI YA MAENEO YA WAZI NA UENDELEZAJI WAKE NCHINI ..... 8

7.0 CHANGAMOTO YA USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA MAENEO YA WAZI ..... 9

8.0 MIKAKATI YA KUTHIBITI UVAMIZI NA MATUMIZI YA MAENEO YA WAZI ..... 10

9.0 MAPENDEKEZO ..... 11

# TAARIFA YA HALI HALISI YA MAENEO YA WAZI NCHINI

## 1.0 UTANGULIZI

Msingi wa ulinzi na uhifadhi wa maeneo ya wazi na maeneo hatarishi unatokana na matamko ya Kisera kupitia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, katika ibara ya 4.3.9 imetambua umuhimu wa maeneo ya wazi, maeneo asili yasiyoendelezwa na maeneo hatarishi kuwa ni muhimu kwa ajili ya kusafisha mzunguko wa hewa na kuondoa muunganiko wa maeneo yaliyoendelezwa au kujengwa. Maeneo ya viwanja vya michezo ya watoto na viwanja vya michezo ni maeneo muhimu sana kwa burudani. Maeneo ya wazi yanapopandwa miti na maua huleta hali ya ukijani na kuboresha mwonekano wa madhari ya mji. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Sera ilielekeza maeneo hayo kulindwa na uvamizi na kuhakikisha yanatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa pekee. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia, Asasi zisizo za kiserikali na Sekta binafsi zitaendeleza maeneo hayo kwa matumizi ya umma. Sera pia iliweka msisitizo wa kutotolewa hati milki ya ardhi kwa wananchi yeyote atakaye vamia maeneo ya wazi na maeneo hatarishi kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000.

Kwa kuzingatia matakwa ya Kisera, Sheria ya Mipangomiji Sura 355 ilizipa jukumu la kupanga, kupima, kutunza na kusimamia maeneo ya wazi Mamlaka za Upangaji nchini kwa kuzingatia mipaka yao ya utawala kwa mujibu wa fungu la 7 (e), (k) na (s) la Sheria ya Mipangomiji Sura ya 355. Hivyo, wakati wa upangaji wa maeneo kupitia upangaji wa maeneo mapya au maeneo ya urasimishaji maeneo hayo hutengwa na kupimwa. Kwa mujibu wa fungu la 15 (1) na (2) la Sheria ya Mipangomiji, Mamlaka husika au taasisi au wamiliki wa ardhi wanaweza kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo yao kwa kuzingatia mpango wa jumla ulioandaliwa katika eneo hilo.

**Sayansi ya usanifu wa miji na maeneo ya wazi** huzingatia kiwango cha Idadi ya watu wanaotarajiwa kuishi katika eneo moja na mgawanyo wa maeneo ya wazi huzingatia uwiano wa eneo kwa mtu, kwa wastani katika eneo la makazi ya watu 100 -150 gawio la ardhi ya eneo la wazi kwa mtu ni mita za mraba 5 hadi 10. Gawio husika linaendelea kupungua kadri kiwango cha upangaji wa mji kinavyoongezeka kuanzia kiunga cha mji (*Neighbourhood; 2-5m$^2$),* Jamii (*community ;1.5-2.5 m$^2$*), Wilaya ya upangaji (*planning district*) (1-2m$^2$) na Jiji au Manispaa (1-2m$^2$ ).Maeneo ya Wazi ni maeneo yaliyopangwa na kuidhinishwa kwa kwa ajili ya matumizi mapana ya Umma yakijumuisha;Mikutano ya hadhara;Mapumziko;Michezo na buradani kwa watoto;kupendezesha mji;Kuhifadhi watu na kutoa misaada katika hali ya dharura au majanga pia kutolea huduma za chanjo za kinga mbalimbali; maeneo ya mikusanyiko maalum; kanda za kijani au Hifadhi ya mazingira mijini.

## 2.0 MATUMIZI YA MAENEO YA WAZI

Kanuni ya 2 ya Kununi ya Udhibiti na Usimamizi wa Maeneo ya Wazi iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na.88 tarehe 9 Marchi, 2018: **Maeneo ya Wazi** ni maeneo yaliyopangwa na kuidhinishwa kwa kwa ajili ya matumizi mapana ya Umma;

Lengo kuu la maeneo ya wazi ni kutumika kwa ajili ustawi wa jamii na mazingira; ikiwepo Maeneo ya kupumzikia, mikusanyiko ya umma ikiwemo mikutano ya hadhara ya mitaa, kuhifadhi watu kwa muda endapo kuna viashiria vya uwezekano wa kutokea kwa athari zinazotokana na majanga ya upepo mkali, mvua kubwa, matetemeko ya ardhi, majanga ya moto na kadhalika (matukio ya dharura).

### 2.1 Umuhimu wa maeneo ya wazi katika miji

#### 2.1.1 Kuongeza Ubora wa Hewa

Maeneo ya wazi yana jukumu muhimu katika kuboresha ubora wa hewa katika miji. Miti na mimea inayopatikana katika maeneo haya husaidia kunyonya kaboni dioksidi na kutoa oksijeni, hivyo kupunguza viwango vya uchafuzi wa hewa. Hii ni muhimu kwa afya ya umma kwani hewa safi inasaidia kupunguza magonjwa yanayohusiana na mfumo wa kupumua.

#### 2.1.2 Kutoa Nafasi za Burudani na kukuza utalii wa ndani

Maeneo ya wazi kama vile parki, viwanja vya michezo, na maeneo ya kupumzikia hutoa nafasi kwa wakazi kujihusisha utalii wa ndani pamoja na shughuli za burudani katika miji husika. Hii inajumuisha michezo, matembezi, maeneo ya kubarizi na shughuli za kijamii ambazo zinachangia kuboresha ustawi wa kimwili na kiakili wa watu. Utafiti umeonyesha kuwa watu wanaofanya mazoezi mara kwa mara katika mazingira ya wazi wanakuwa na afya bora. Hivyo maneo ya wazi yaliyoendelezwa na kuboreshwa kwa kuwekewa miundombinu ya huvutia jamii katika kuyatumia na kuongeza hamasa ya kutumika kwa michezo na mazoezi mbalimbali hivyo kimarisha afya za wakazi mijini.

#### 2.1.3 Kuhifadhi Biodiversity

Maeneo ya wazi ni muhimu kwa kuhifadhi aina mbalimbali za mimea na wanyama. Kwa kuwepo kwa mazingira yasiyo ya asilia kama vile misitu, mabwawa, na maeneo mengine yasiyoguswa, miji inaweza kusaidia kulinda viumbe hai vinavyotegemea mazingira haya kwa ajili ya kuishi. Hii ina umuhimu mkubwa katika kudumisha mfumo wa ikolojia ambao unasaidia maisha yote. Pia husaidia katika kuimarisha suala zima la kuwa na miji iliyopangwa sambamba na maumbile yenye mwonekano wa kijani kibichi yenye mvuto kimazingira.

#### 2.1.4 Kuimarisha Jamii

Maeneo ya wazi yanatoa fursa kwa jamii kukutana na kuungana. Matukio kama vile mikutano ya hadhara, makongamano, masoko ya wakulima, matamasha, na shughuli za kijamii zinaweza kufanyika katika maeneo haya, hivyo kuimarisha uhusiano kati ya

wanajamii. Ushirikiano huu unachangia kujenga jamii zenye nguvu zaidi ambazo zinaweza kushirikiana katika kutatua changamoto zinazowakabili.

### 2.1.5 Kuongeza Thamani ya Mali na kuvutia uwekezaji

Uwepo wa maeneo ya wazi huongeza thamani ya mali katika eneo husika. Watu wengi wanapendelea kuishi karibu na maeneo haya kutokana na faida zao za kiafya na kijamii, hivyo kuongeza bei za ardhi na nyumba karibu nao. Hii inachangia ukuaji wa kiuchumi katika miji ikiwepo na kutoa fursa ya kuvutia uwekezaji katika kuendeleza miji ya kisasa.

### 2.1.6 Kusaidia Katika Usimamizi wa Maji

Maeneo ya wazi yanaweza kusaidia katika usimamizi wa maji ya mvua kupitia mifumo kama vile mabwawa au maeneo yenye majani ambayo yanaruhusu maji kunyeshewa ardhini badala ya kusababisha mafuriko. Hii ni muhimu hasa katika miji ambapo miundombinu inaweza kuwa duni au isiyoweza kushughulikia mvua nyingi.

Kwa ujumla, umuhimu wa maeneo ya wazi hauwezi kupuuziliwa mbali; maeneo hayo yana mchango mkubwa si tu katika kuboresha mazingira bali pia katika ustawi wa jamii nzima na kuboresha madhari ya miji nchini.

## 3.0 MADHARA YA KUKOSEKANA KWA MAENEO YA WAZI

Kuna athari zinazojitokeza za kijamii, kiuchumi na kimazingira kutokana na kukosekana kwa maeneo ya wazi katika miji. Athari hizo ni pamoja na:-

### 3.1 Athari za Kijamii

Kukosekana kwa maeneo ya wazi katika miji kunaweza kuathiri sana maisha ya kijamii. Maeneo haya yanatoa nafasi kwa watu kukutana, kuzungumza, na kushiriki katika shughuli za kijamii. Bila maeneo haya, kuna uwezekano wa kupungua kwa ushirikiano wa jamii na kuongezeka kwa hali ya upweke na kutengwa. Hali hii inaweza kusababisha ongezeko la matatizo ya afya ya akili kama vile wasiwasi na unyogovu. Pia kudhoofisha dhana au mikakati ya kuijenga jamii yenye kushirikiana katika kujiletea maendeleo katika maeneo husika.

### 3.2 Athari za Kiafya

Maeneo wazi yana umuhimu mkubwa katika kuboresha afya ya umma. Yanatoa nafasi kwa watu kufanya mazoezi, kupumzika, na kufurahia mazingira asilia. Kukosekana kwa maeneo haya kunaweza kuongeza kiwango cha ukosefu wa shughuli za mwili, hivyo kupelekea ongezeko la magonjwa yasiyoyo yakuambukiza kama vile kisukari, ugonjwa wa moyo, na fetma. Aidha, maeneo yasiyo na hewa safi yanaweza kusababisha matatizo ya mfumo wa kupumua.

### 3.3 Athari za Kimazingira

Maeneo wazi ni muhimu katika kudumisha mazingira bora katika miji. Yanasaidia katika kudhibiti joto la mji, kutoa kivuli, na kusaidia katika uhifadhi wa maji mvua. Kukosekana kwa maeneo haya kunaweza kusababisha ongezeko la joto la mijini (urban heat island effect), ambapo joto linakuwa juu zaidi kuliko maeneo ya vijijini. Pia, kukosekana kwa nafasi hizi kunaweza kupelekea uharibifu wa bioanuwai kwani viumbe hai wanahitaji maeneo wazi ili kuishi.

### 3.4 Athari za Kiuchumi

Maeneo wazi yanaweza kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa mitaa kupitia utalii na biashara zinazohusiana na burudani. Kukosekana kwa maeneo haya kunaweza kupunguza fursa za ajira zinazohusiana na sekta hizi, hivyo kuathiri uchumi wa eneo hilo. Aidha, miji isiyo na maeneo wazi inaweza kuwa vigumu kuvutia wawekezaji au wakazi wapya ambao wanatafuta mazingira bora ya kuishi.

### 3.5 Athari za Utamaduni

Maeneo wazi mara nyingi huwa ni sehemu muhimu za utamaduni wa jamii fulani. Wanatoa fursa kwa matukio mbalimbali kama vile sherehe za kitamaduni, maonyesho ya sanaa, na mikutano ya kijamii ambayo inachangia katika utambulisho wa jamii hiyo. Kukosekana kwa nafasi hizi kunaweza kusababisha upungufu wa utamaduni na urithi wa jamii.

Kwa ujumla, kukosekana kwa maeneo wazi katika miji kuna madhara mengi ambayo yanahusiana moja kwa moja na ustawi wa jamii, afya ya umma, mazingira, uchumi, na utamaduni.

## 4.0 USIMAMIZI NA UDHIBITI WA MAENEO YA WAZI

Maeneo ya wazi nchini husimamiwa kwa mujibu wa Sera, Sheria na Kanuni zinazongoza matumizi na usimamizi wa maeneo hayo zikiwemo;

- Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 fungu la 6 .6.0 (i-ii), Sera ya Maendeleo ya Makazi 4(3) na fungu la 28 (f) la Sheria ya Mipangomiji. Vyote hivi vinaeleza umuhimu wa maeneo ya wazi mijini na kuhimiza yalindwe na kudumishwa.
- Kwa mujibu wa fungu la 28 (f) la Sheria ya Mipangomiji, mamlaka za upangaji nchini zimepewa jukumu la kuyasimamia na kuyahifadhi na bila kuathiri matumizi ya maeneo hayo.
- Pia, fungu la 4-7 la Kanuni za Sheria ya Mipangomiji za mwaka 2018 (Uthibiti na Usimamizi wa maeneo ya umma) zilizotangazwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 88 la mwaka 2018 imetoa utaratibu wa uthibiti na usimamizi wa maeneo hayo ikiwemo kuyatoa kwa taasisi, mtu binafsi au kikundi kwa ajili ya kuendeleza na

kuyasimamia, kuyawekea uzio na kutoa masharti ya uendelezaji endapo itayakodisha kwa waendelezaji binafsi/taasisi/vikundi/jamii.

- Kanuni Na. 6(3)(a) ya Kanuni za Viwango vya Upangaji kwa matumizi ya Ardhi iliyochapishwa katika gazeti la serikali Na. 91 mwaka 2018 inazuia kabisa, kubadilisha matumizi ya maeneo ya wazi.

Kwa mantiki hiyo, maeneo hayo yanasimamiwa na Halmashauri husika lakini yanaweza kutunzwa na mtu binafsi, vikundi au jamii kwa makubaliano maalum au mikataba na halmashauri husika. Hivyo, maeneo hayo hayaendelezwi kwa ujenzi wa majengo ya kudumu au kuwekea vizuizi vitakavyopelekea watu kushindwa kuyatumia maeneo hayo kama ilivyokusudiwa.

**Aidha, wizara imefanya mapendekezo ya maboresho ya kanuni za mipango miji na kuongeza**

i. Aina ya umiliki wa maeneo ya wazi: Ambapo kutakuwa na maeneo yatakayomilikiwa na watu binafsi yanayotokana na ardhi binafsi ya mtu baada ya halmashauri kushindwa kuyakomboa kwa kulipa fidia kwa wamiliki wa maeneo hayo, na yatakayomilikiwa na serikali yanatokana na utwaaji wa ardhi.

ii. Waziri wa Ardhi, kupewa dhamana ya kubadilisha matumizi ya maeneo ya wazi pale hitaji linapotokea na mabadiliko haya yataidhinishwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi iwapo tu atajiridhisha kuwa kuna manufaa makubwa ya umma katika kutumia eneo la wazi.

## 5.0 UTARATIBU WA KUPANGISHA MAENEO YA WAZI

Kulingana na Kanuni iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 88 ya sheria ya Mipangomiji (Usimamizi na udhibiti wa maeneo ya wazi ya umma) imetoa utaratibu ufuatao katika kupangisha/kutumia maeneo ya wazi

- Mamlaka ya upangaji inaruhusiwa kutoa kibali cha kuendeleza, kutunza eneo la wazi la umma kwa mtu, kikundi cha watu au Taasisi
- Hairuhusiwi kujenga majengo ya kudumu isipokuwa vyoo
- Muda wa kukodishwa ni miaka 1-5 ambayo inaweza kuhuishwa
- Katika hali ya utendaji usioridhishwa, Mamlaka ya upangaji au Mkurugenzi anaweza kusitisha kibali baada ya notisi ya siku 14
- Mamlaka ya upangaji inaruhusiwa kutoa masharti yoyote ya uendelezaji na utumiaji yasiyokuwa na lengo la kuondoa matumizi msingi ya eneo husika.

## 6.0 HALI YA MAENEO YA WAZI NA UENDELEZAJI WAKE NCHINI

### 6.1. Hali ya maeneo ya wazi

Wizara inajukumu muhimu la kusimamia Sera, Sheria na Kanuni za Uendelezaji wa Miji. Aidha, Sera ya Maendeleo ya Makazi ibara ya 4.3.9 inatamka umuhimu wa maeneo ya wazi mijini na kuzuia maeneo hayo kuendelezwa kinyume na makusudio ikiwepo na kuzuia kabisa wavamizi wa maeneo, kumilikishwa na kupatiwa hati.

Kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa mwezi Septamba, 2024, kupitia Ofisi za Ardhi za Mikoa 26 kwa kuhusisha Mamlaka za Upangaji(Halmashauri) 178 nchini zilizowasilisha taarifa zake; umebaini kuwepo kwa jumla ya maeneo ya wazi ya umma **34,689** yenye ukubwa wa hekta **24,487.19** ambayo yameidhinishwa kupitia michoro ya mipangokina iliyoandaliwa katika miji. Kati ya hayo, maeneo ya 10,237 yamefanyiwa upimaji ambapo **8,980** yamelipiwa fidia. Aidha, kati ya maeneo yote yaliyoainishwa maeneo **1,709** sawa na 4.93 % yameendelezwa kinyume na matumizi yaliyokusudiwa.

Pamoja na hayo, mkoa wa Kigoma unaongoza kwa asilimia 37.85 ya uvamizi/uendelezaji wa maeneo ya wazi kinyume na matumizi yaliyokusudiwa ukifuatiwa na mkoa wa Geita (26.34%), Mara (24.4%) na Kagera (14.52%)

Kwa upande wa majiji hali ya uvamizi umeshamiri zaidi katika jiji la Mwanza (8.01%), na kufuatiwa na jiji la Mbeya (7.16%), Dar es Salaam (4.22%), Dodoma (2.99%) na Arusha (1.41%)**(Tazama Jedwali Na. 1).**

Aidha, Wizara inashauri mamlaka za upangaji(Halmashauri) zinazomiliki maeneo ya wazi hayo **1,709** kuangalia taratibu za kuyakomboa maeneo hayo kwa njia zifuatazo;

i. Kuandaa notisi na kuwaondoa wavamizi;

ii. Kuinisha maeneo yote ya wazi yaliyo katika maeneo yao ya kiutawala na kuyafanyia tathmini ya kina kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuyalinda na kuyaendeleza kwa manufaa mapana ya matumizi ya umma;

iii. Kulipa fidia kwa wamilki wa ardhi katika maeneo ya wazi ili yawe huru kwa matumizi yaliyokusudiwa;

iv. Maeneo ya wazi yote yaliyosanifiwa kupitia michoro ya mipangomiji yapimwe na halmashauri hizo kumilikishwa maeneo hayo ya umma ikiwepo nay ale ambayo tayari upimaji wake umefanyika ili kuyalinda.

### 6.2. Hali ya uendelezaji wa maeneo ya wazi

Katika kuhakikisha maeneo ya wazi yanaendelezwa kwa makusudio yaliyopangwa. Wizara ilitunga Kanuni za Sheria ya Mipangomiji Sura ya 355 ambazo zilichapishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 88 la mwaka 2018. Pamoja na uwepo wa kanuni hizo ambazo zinatoa fursa kwa Mamlaka za Upangaji kuyaendeleza maeneo hayo kwa

makusudio yaliyopangwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali bado hali ya uendelezaji wa maeneo hayo haijatiliwa mkazo na hivyo kuyafanya kupoteza umuhimu wake mijini. Jitihada kubwa zimekuwa zikifanyika za kutenga maeneo hayo kwa lengo la kuifanya miji yetu kuwa endelevu na rafiki kwa jamii, kimazingira na kiuchumi.

Hali ya uendelezaji na utunzaji wa maeneo ya wazi na burudani nchini ni chini sana na inatofautiana katika majiji na halmashauri mbalimbali nchini. Mfano, kwa upande wa majiji, Jiji la Dodoma ni maeneo ya wazi 6 tu ndiyo yameendelezwa kati ya maeneo ya wazi 2,862 sawa asilimia 0.2 ya yaliyobuniwa kupitia michoro ya mipangamiji katika Jiji hilo. Aidha, Jiji la Mwanza limeendeleza maeneo maeneo ya wazi 4 kati ya maeneo 312 sawa na asilimia 1,3, Jiji la Dar es Salaam limeendeleza maeneo 11 kati ya maeneo 542 sawa na asilimia 2, Arusha imeendeleza maeneo 10 kati ya maeneo 205 sawa na asilimia 4.9 na Mbeya iliendeleza maeneo 2 kati ya maeneo 112 sawa na salimia 1.7.

Kimsingi hali ya uendelezaji wa maeneo ya wazi nchini hairidhishi na badala yake maeneo hayo yametelekezwa na Mamlaka za Upangaji na hayapewi kipaumbele cha cha kutosha katika mipango ya maendeleo ya mamlaka za upangaji ya kila mwaka hivyo kuifanya miji kutokuwa rafiki kijamii, kimazingira na kiuchumi na kupelekea uwepo wa miji isiyokuwa na mvuto ukilinganisha na miji mingine duniani. Aidha, kutokuendelezwa na kutelekezwa kwa maeneo hayo kunavutia na kushawishi uvamizi wa maeneo hayo ikiwepo na mamlaka zenyewe kuanzisha michakato ya kuyaombea mabadiliko ya matumizi ambayo ni kinyume na Sera na Sheria ambazo zimezuia kabisa maeneo hayo kufanyika mabadiliko.

## 7.0 CHANGAMOTO YA USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA MAENEO YA WAZI

Uchunguzi uliofanyika katika Mamlaka za Upangaji umebaini kuwa miongoni mwa changamoto zinazosabisha kuendelezwa na kutumiwa kwa maeneo hayo kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu ni zifuatazo: -

i. Baadhi ya Maeneo yaliyobuniwa kutumika kwa matumizi ya wazi kutotwaliwa na kulipiwa fidia kwa mujibu wa Sheria, hivyo kutoa fursa kwa wamilki wa asili kuyamega na kuyauza kwa waendelezaji mbalimbali;

ii. Baadhi ya maeneo kuvamiwa kwa makusudi, kutumiwa vinginevyo na baadhi ya wananchi wasio waaminifu kuyaendeleza kwa ujenzi wa majengo ya kudumu;

iii. Baadhi ya Mamlaka za Upangaji kupitia vikao halali vya kudumu vya Halmashauri kubadili matumizi na kugawa maeneo ya wazi kwa matumizi mengine kwa madai kuwa ni kipaumbele ni kutafuta mapato na maeneo hayo ni mali yao; Mfano Halmashauri ya Kigoma Ujiji iligawa maeneo ya wazi mjini, lakini ilizuiliwa na wizara;

iv. Baadhi ya Mamlaka mbalimbali kwa nyakati tofauti kugawa maeneo ya wazi na kuyabadilisha matumizi kwa ajili ya matumizi mengine ya umma, yakiwemo shule, ofisi za serikali, vituo vya afya ikiwepo na Taasisi za dini na zile za kisiasa kuyaendeleza kinyume cha sheria;

v. Baadhi ya watalaam wa sekta ya ardhi wasio waaminifu (Maafisa Mipangomiji, Maafisa ardhi na Wapima ardhi) kubadili matumizi, kupima na kumilikisha maeneo ya wazi kwa matumizi mengine;

vi. Baadhi ya maeneo ya wazi serikali inashindwa kulipia fidia na kusababisha wenye ardhi kuyaendeleza vinginevyo;

vii. Maeneo mengi ya wazi naya burudani kuachwa bila kuendelezwa kwa matumizi ya umma;

viii. Maeneo ya wazi kutokupimwa na kumilikishwa kwa mamlaka za upangaji

## 8.0 MIKAKATI YA KUTHIBITI UVAMIZI NA MATUMIZI YA MAENEO YA WAZI

Kutokana na changamoto hizo, Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 kupitia tamko Na. 4.3.9.2 imetamka kuwa Serikali itahakikisha kuwa maeneo ya wazi, maeneo ya burudani na maeneo hatarishi yanalindwa dhidi ya uvamizi na yanatumika kwa shughuli iliyopangwa; Mamlaka za upangaji, vikundi vya kijamii, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi binafsi na umma zinayaendeleza maeneo ya wazi na maeneo ya burudani kwa manufaa ya umma; na Hayatamilikishwa kwa watu/mtu atakayevamia maeneo ya wazi, maeneo hatarishi na maeneo ya hifadhi:

i. Wizara kwa nyakati tofauti tofauti imekuwa ikiziandikia mamlaka za upangaji kuzingatia Sera na Sheria za Usimamizi wa Maeneo ya Wazi;

ii. Wizara kwa vipindi tofauti imekuwa ikishirikana na halmashauri husika kuzuia uvamizi wa maeneo ya wazi pale inapopata taarifa za haraka za uvamizi;

iii. Kupitia miradi yote ya upangaji na upimaji ardhi inayosimamiwa na wizara upatikanaji wa maeneo ya wazi na burudani yanapatikana na kuhifadhiwa/kuendelezwa kwa kuzingatia sheria/taratibu zilizopo ili kuepuka uvamizi na migogoro. Mfano mradi wa KKK na LTIP maeneo yote ya matumizi ya umma yamepatikana kwa kuzingatia sheria/utaratibu ili kuepuka uvamizi wa maeneo hayo.

## 9.0 MAPENDEKEZO

Ili kudhibiti uvamizi, mabadiliko ya matumizi ya ardhi na uendelezaji wa maeneo ya wazi kinyume na sheria, Kanuni na Taratibu yafuatayo yanapendekezwa;

i. Mamlaka za upangaji zielekezwe kujumuisha suala la uendelezaji wa maeneo ya wazi kwenye mipango yake ya maendeleo ya kila mwaka ili kuboresha madhari ya miji na kuimarisha huduma ya matumizi ya maeneo hayo kwa jamii;

ii. Viongozi ngazi ya kata na mitaa husika washirikishwe kuyatambua, kuyalinda, kuyatunza na kuyatumia kwa madhumuni husika. Mamlaka za upangaji ziandae na kugawa michoro na ramani katika mitaa na kata na kuwagawia na kuwafundisha namna ya kuzitafsiri na kuzitumia ramani hizo,

iii. Mamlaka za upangaji ziyapime, zimiliki, ziyalinde na kuyatunza kwa Mujibu wa Sheria Maeneo ya wazi na kuchukua hatua stahiki kwa matumizi yoyote kinyume na mipango;

iv. Mamlaka za Upangaji zitumie mabango yenye ujumbe wa kuyatambulisha maeneo ya Wazi unaosomeka kirahisi na wananchi;

v. Mamlaka za upangaji zijenge uzio usio wa kudumu au kuweka nguzo zinazoonekana kwa ajili ya kuyalinda maeneo ya Wazi;

vi. Mamlaka ya Upangaji nchini zishirikishe kikamilifu sekta binafsi juu ya uendelezaji wa maeneo ya wazi kwa madhumuni yaliyokusudiwa na fursa zilizopo katika sheria ya usimamizi na matumizi ya maeneo hayo

## JEDWALI Na. 1: TAARIFA YA HALI HALISI YA MAENEO YA WAZI NCHINI

| Na | MIKOA | HALMASHAURI | MAENEO YA WAZI | | HALI HALISI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | IDADI | UKUBWA (Ha) | YALIYO FIDIWA | YALIYO PIMWA | UVAMIZI | % YA UVAMIZI |
| 1 | Arusha | Arusha District Council | 248 | 144.32 | 23 | 23 | 0 | 0 |
| | | Arusha City Council | 205 | 106.04 | 48 | 48 | 0 | 0 |
| | | Karatu District Council | 98 | 110.51 | 24 | 22 | 0 | 0 |
| | | Longido District Council | 53 | 113.89 | 8 | 8 | 11 | 20.75 |
| | | Meru District Council | 190 | 161.30 | 18 | 18 | 0 | 0 |
| | | Monduli District Council | 114 | 81.81 | 12 | 12 | 2 | 1.75 |
| | | Ngorongoro District Council | 19 | 7.93 | 11 | 6 | 0 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **927** | **725.80** | **144** | **137** | **13** | **1.41** |
| | | | | | | | | |
| 2 | Dar es Salaam | Ilala Municipal Council | 542 | 294.38 | 118 | 58 | 8 | 1.47 |
| | | Kinondoni Municipal Council | 343 | 220.88 | 0 | 139 | 59 | 17.21 |
| | | Ubungo Municipal Council | 328 | 121.21 | 3 | 328 | 31 | 9.45 |
| | | Temeke Municipal Council | 146 | 60.08 | 146 | | 14 | 9.58 |
| | | Kigamboni Municipal Council | 1295 | 1071.11 | 156 | 133 | 0 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **2654** | **1767.66** | **423** | **658** | **112** | **4.22** |
| | | | | | | | | |
| 3 | Dodoma | Chemba District Council | 31 | 34.23 | 9 | 30 | 3 | 9.68 |
| | | Bahi District Council | 56 | 30.78 | 7 | 21 | 2 | 3.57 |
| | | Kongwa District Council | 248 | 155.22 | 32 | 54 | 3 | 1.21 |
| | | Kondoa District Council | 11 | 8.01 | 4 | 8 | 0 | 0 |
| | | Kondoa Town Council | 69 | 80.94 | 24 | 32 | 3 | 4.34 |
| | | Mpwapwa District Council | 121 | 87.16 | 22 | 25 | 1 | 0.83 |
| | | Chamwino District Council | 342 | 191.62 | 69 | 78 | 9 | 2.63 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Dodoma City Council | 2862 | 3,293.45 | 1468 | 2146 | 91 | 3.18 |
| | | **Jumla Ndogo** | **3740** | **3881.41** | **1635** | **2394** | **112** | **2.99** |
| | | | | | | | | |
| 4 | Geita | Geita District Council | 138 | 88.97 | 12 | 27 | 93 | 67.39 |
| | | Bukombe District Council | 129 | 141.29 | 12 | 10 | 48 | 37.21 |
| | | Chato District Council | 150 | 149.24 | 25 | 24 | 46 | 30.67 |
| | | Geita Town Council | 292 | 242.17 | 26 | 26 | 3 | 1.03 |
| | | Mbogwe District Council | 55 | 63.35 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | Nyang'hwale District Council | 94 | 159.55 | 41 | 11 | 36 | 38.3 |
| | | **Jumla Ndogo** | **858** | **844.57** | **116** | **98** | **226** | **26.34** |
| | | | | | | | | |
| 5 | Iringa | Iringa MC | 438 | 283.16 | 24 | 24 | 8 | 1.83 |
| | | Iringa DC | 138 | 81.57 | 16 | 16 | 28 | 20.29 |
| | | Kilolo DC | 55 | 32.79 | 10 | 10 | 15 | 27.27 |
| | | Mafinga TC | 320 | 161.26 | 22 | 22 | 21 | 6.56 |
| | | Mufindi DC | 53 | 20.80 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **1004** | **579.58** | **73** | **73** | **72** | **7.17** |
| | | | | | | | | |
| 6 | Kagera | Muleba District Council | 195 | 128.98 | 39 | 36 | 2 | 1.03 |
| | | Missenyi District Council | 70 | 67.58 | 14 | 14 | 4 | 5.71 |
| | | Bukoba Municipal Council | 53 | 24.42 | 27 | 28 | 1 | 1.89 |
| | | Biharamulo District Council | 95 | 82.34 | 8 | 12 | 3 | 3.16 |
| | | Bukoba District Council | 66 | 22.74 | 10 | 17 | 5 | 7.58 |
| | | Karagwe District Council | 61 | 25.26 | 63 | 4 | 61 | 100 |
| | | Kyerwa District Council | 33 | 19.69 | 9 | 9 | 2 | 6.06 |
| | | Ngara District Council | 26 | 15.06 | 0 | 18 | 8 | 30.77 |
| | | **Jumla Ndogo** | **599** | **386.07** | **170** | **138** | **87** | **14.52** |
| | | | | | | | | |
| 7 | Katavi | Nsimbo District Council | 113 | 72.02 | 17 | 17 | 0 | 0 |
| | | Mpanda District Council | 144 | 362.62 | 0 | 0 | 0 | 0 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mlele District Council | 38 | 11.45 | 16 | 16 | 0 | 0 |
| | | Mpimbwe District Council | 24 | 42.29 | 10 | 10 | 0 | 0 |
| | | Mpanda Municipal Council | 364 | 230.80 | 21 | 21 | 5 | 1.37 |
| | | Tanganyika District Council | 39 | 10.13 | 33 | 33 | 5 | 12.82 |
| | | **Jumla Ndogo** | **683** | **729.31** | **97** | **97** | **10** | **1.46** |
| | | | | | | | | |
| 8 | Kigoma | Buhigwe District Council | 21 | 15.01 | 25 | 25 | 6 | 28.57 |
| | | Kakonko District Council | 25 | 1.97 | 25 | 25 | 6 | 24.0 |
| | | Kasulu District Council | 14 | 3.53 | 14 | 7 | 14 | 100 |
| | | Kasulu Town Council | 40 | 44.39 | 40 | 13 | 14 | 35 |
| | | Kibondo District Council | 26 | 29.82 | 14 | 12 | 12 | 46.15 |
| | | Kigoma District Council | 75 | 55.90 | 27 | 10 | 27 | 36 |
| | | Kigoma Ujiji Municipal Council | 111 | 104.61 | 103 | 82 | 57 | 51.35 |
| | | Uvinza District Council | 108 | 31.91 | 108 | 30 | 23 | 21.3 |
| | | **Jumla Ndogo** | **420** | **287.14** | **356** | **204** | **159** | **37.86** |
| | | | | | | | | |
| 9 | Kilimanjaro | Hai District Council | 78 | 151.49 | 58 | 24 | 2 | 2.56 |
| | | Siha District Council | 103 | 122.38 | 68 | 26 | 0 | 0 |
| | | Moshi District Council | 159 | 202.76 | 73 | 13 | 8 | 5.03 |
| | | Moshi Municipal Council | 55 | 17.28 | 115 | 29 | 21 | 38.18 |
| | | Mwanga District Council | 132 | 155.70 | 19 | 22 | 16 | 12.12 |
| | | Rombo District Council | 49 | 103.62 | 33 | 5 | 3 | 6.12 |
| | | Same District Council | 61 | 51.14 | 52 | 0 | 3 | 4.92 |
| | | **Jumla Ndogo** | **637** | **804.37** | **418** | **119** | **53** | **8.32** |
| | | | | | | | | |
| 10 | Lindi | Nachingwea District Council | 149 | 76.07 | 23 | 31 | 8 | 5.37 |
| | | Mtama District Council | 85 | 212.23 | 15 | 11 | 0 | 0 |
| | | Lindi Municipal Council | 504 | 334.28 | 43 | 43 | 0 | 0 |
| | | Kilwa District Council | 178 | 176.19 | 8 | 11 | 1 | 0.56 |
| | | Ruangwa District Council | 124 | 61.35 | 11 | 11 | 0 | 0 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Liwale District Council | 93 | 41.05 | 11 | 15 | 1 | 1.08 |
| | | **Jumla Ndogo** | **1133** | **901.17** | **111** | **122** | **10** | **0.88** |
| | | | | | | | | |
| 11 | Manyara | Kiteto District Council | 41 | 28.54 | 3 | 4 | 1 | 2.44 |
| | | Babati Town Council | 333 | 172.41 | 21 | 67 | 4 | 1.2 |
| | | Mbulu District Council | 61 | 27.67 | 0 | 20 | 1 | 1.64 |
| | | Mbulu Town Council | 52 | 35.80 | 0 | 6 | 5 | 9.61 |
| | | Simanjiro District Council | 121 | 99.49 | 2 | 5 | 3 | 2.48 |
| | | Babati District Council | 113 | 61.87 | 5 | 5 | 0 | 0 |
| | | Hanang District Council | 115 | 132.58 | 22 | 22 | 0 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **836** | **558.36** | **53** | **129** | **14** | **1.67** |
| | | | | | | | | |
| 12 | Mara | Bunda District Council | 37 | 21.67 | 0 | 3 | 6 | 16.21 |
| | | Bunda Town Council | 233 | 217.51 | 64 | 66 | 98 | 42.06 |
| | | Musoma District Council | 48 | 49.09 | 2 | 5 | 9 | 18.75 |
| | | Musoma Municipal Council | 200 | 296.01 | 8 | 53 | 8 | 4 |
| | | Serengeti District Council | 71 | 56.18 | 23 | 33 | 7 | 9.86 |
| | | Rorya District Council | 59 | 56.90 | 8 | 10 | 12 | 20.34 |
| | | Tarime District Council | 49 | 36.55 | 0 | 6 | 21 | 42.86 |
| | | Tarime Town Council | 76 | 21.24 | 0 | 27 | 26 | 34.21 |
| | | Butiama District Council | 55 | 35.55 | 0 | 12 | 6 | 10.91 |
| | | **Jumla Ndogo** | **791** | **769.03** | **105** | **215** | **193** | **24.4** |
| | | | | | | | | |
| 13 | Mbeya | Chunya District Council | 57 | 43.23 | 0 | 18 | 1 | 1.75 |
| | | Kyela District Council | 54 | 27.66 | 8 | 8 | 0 | 0 |
| | | Mbarali District Council | 168 | 100.24 | 0 | 17 | 1 | 0.59 |
| | | Mbeya City Council | 112 | 4.33 | 110 | 131 | 32 | 28.57 |
| | | Mbeya District Council | 49 | 30.89 | 10 | 10 | 0 | 0 |
| | | Busokelo District Council | 48 | 4.01 | 0 | 9 | 7 | 14.58 |
| | | Rungwe District Council | 85 | 57.99 | 23 | 7 | 0 | 0 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Jumla Ndogo** | **573** | **268.35** | **151** | **200** | **41** | **7.16** |
| | | | | | | | | |
| 14 | Morogoro | Gairo District Council | 63 | 30.11 | 16 | 15 | 1 | 1.59 |
| | | Ifakara Town Council | 140 | 65.21 | 16 | 16 | 6 | 4.29 |
| | | Kilombero/Mlimba District Council | 30 | 13.90 | 6 | 6 | 0 | 0 |
| | | Kilosa District Council | 310 | 338.57 | 56 | 76 | 8 | 2.58 |
| | | Malinyi District Council | 34 | 8.71 | 7 | 7 | 0 | 0 |
| | | Morogoro District Council | 119 | 96.90 | 53 | 66 | 12 | 10.08 |
| | | Morogoro Municipal Council | 890 | 1063.75 | 260 | 322 | 100 | 11.23 |
| | | Mvomero District Council | 420 | 205.34 | 119 | 132 | 6 | 1.43 |
| | | Ulanga District Council | 47 | 23.54 | 2 | 14 | 2 | 4.26 |
| | | **Jumla Ndogo** | **2053** | **1846.03** | **529** | **654** | **135** | **6.58** |
| | | | | | | | | |
| 15 | Mtwara | Nanyumbu District Council | 63 | 40.26 | 63 | 63 | 0 | 0 |
| | | Masasi District Council | 79 | 43.73 | 0 | 6 | 1 | 1.27 |
| | | Masasi Town Council | 154 | 94.54 | 122 | 153 | 8 | 5.19 |
| | | Mtwara District Council | 273 | 176.97 | 19 | 273 | 0 | 0 |
| | | Mtwara Municipal Council | 437 | 277.86 | 425 | 425 | 2 | 0.46 |
| | | Nanyamba Town Council | 66 | 23.86 | 8 | 49 | 0 | 0 |
| | | Newala District Council | 24 | 25.35 | 0 | 3 | 2 | 8.33 |
| | | Newala Town Council | 126 | 77.10 | 28 | 28 | 5 | 9.97 |
| | | Tandahimba District Council | 79 | 44.43 | 23 | 30 | 3 | 3.8 |
| | | **Jumla Ndogo** | **1301** | **804.10** | **688** | **1030** | **21** | **1.61** |
| | | | | | | | | |
| 16 | Mwanza | Misungwi District Council | 308 | 163.38 | 148 | 66 | 22 | 7.14 |
| | | Ukerewe District Council | 41 | 25.45 | 21 | 28 | 86 | 19.51 |
| | | Sengerema District Council | 185 | 164.25 | 15 | 15 | 5 | 2.7 |
| | | Buchosa District Council | 26 | 18.48 | 31 | 0 | 0 | 0 |
| | | Magu District Council | 245 | 209.47 | 48 | 35 | 11 | 4.49 |
| | | Kwimba District Council | 141 | 86.83 | | 18 | 6 | 4.26 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ilemela Municipal Council | 1164 | 2260 | 891 | 1164 | 29 | 2.49 |
| | | Mwanza City Council | 312 | 319.29 | 8 | 66 | 35 | 11.21 |
| | | **Jumla Ndogo** | **2422** | **3247.15** | **1179** | **1392** | **194** | **8.01** |
| | | | | | | | | |
| 17 | Njombe | Ludewa District Council | 19 | 9.92 | 19 | 3 | 0 | 0 |
| | | Njombe District Council | 82 | 39.93 | 8 | 9 | 0 | 0 |
| | | Makambako Town Council | 287 | 180.15 | 0 | 60 | 19 | 6.62 |
| | | Njombe Town Council | 198 | 127.13 | 190 | 37 | 11 | 5.56 |
| | | Makete District Council | 24 | 13.67 | 4 | 6 | 1 | 4.17 |
| | | Wanging'ombe District Council | 138 | 73.82 | 68 | 6 | 1 | 0.72 |
| | | **Jumla Ndogo** | **748** | **444.62** | **289** | **121** | **32** | **4.28** |
| | | | | | | | | |
| 18 | Pwani | Kisarawe District Council | 528 | 221.54 | 17 | 17 | 0 | 0 |
| | | Kibiti District Council | 264 | 72.79 | 246 | 30 | 0 | 0 |
| | | Bagamoyo District Council | 886 | 666.18 | 27 | 124 | 13 | 1.47 |
| | | Chalinze District Council | 717 | 327.47 | 33 | 99 | 1 | 0.14 |
| | | Kibaha District Council | 489 | 264.69 | 42 | 57 | 2 | 0.41 |
| | | Kibaha Town Council | 576 | 362.57 | 18 | 37 | 4 | 0.69 |
| | | Mafia District Council | 114 | 183.31 | 2 | 28 | 0 | 0 |
| | | Rufiji District Council | 191 | 212.58 | 20 | 3 | 1 | 0.52 |
| | | Mkuranga District Council | 1134 | 584.32 | 9 | 10 | 0 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **4881** | **2895.45** | **414** | **405** | **21** | **0.43** |
| | | | | | | | | |
| 19 | Rukwa | Kalambo District Council | 98 | 62.51 | 23 | 23 | 0 | 0 |
| | | Nkasi District Council | 76 | 55.46 | 26 | 25 | 1 | 1.32 |
| | | Sumbawanga District Council | 61 | 20.44 | 11 | 11 | 0 | 0 |
| | | Sumbawanga Municipal Council | 269 | 174.80 | 101 | 101 | 12 | 4.46 |
| | | **Jumla Ndogo** | **504** | **313.21** | **161** | **160** | **13** | **2.58** |
| | | | | | | | | |
| 20 | Ruvuma | Mbinga District Council | 542 | 187.17 | 99 | 99 | 5 | 0.92 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mbinga Town Council | 231 | 67.57 | 69 | 182 | 3 | 1.3 |
| | | Namtumbo District Council | 135 | 72.71 | 40 | 40 | 4 | 2.96 |
| | | Nyasa District Council | 78 | 38.05 | 23 | 23 | 3 | 3.85 |
| | | Madaba District Council | 96 | 44.44 | 29 | 29 | 1 | 1.04 |
| | | Songea District Council | 143 | 140.93 | 32 | 33 | 1 | 0.7 |
| | | Songea Municipal Council | 609 | 180.53 | 169 | 182 | 1 | 0.16 |
| | | Tunduru District Council | 137 | 58.08 | 35 | 37 | 2 | 1.46 |
| | | **Jumla Ndogo** | **1614** | **784.48** | **496** | **625** | **20** | **1.24** |
| | | | | | | | | |
| 21 | Shinyanga | Kishapu District Council | 57 | 68.21 | 8 | 8 | 0 | 0 |
| | | Msalala District Council | 354 | 134.35 | 103 | 28 | 2 | 0.56 |
| | | Ushetu District Council | 59 | 33.78 | 3 | 3 | 0 | 0 |
| | | Kahama Municipal Council | 374 | 213.88 | 15 | 55 | 3 | 0.8 |
| | | Shinyanga District Council | 60 | 62.32 | 4 | 11 | 0 | 0 |
| | | Shinyanga Municipal Council | 83 | 57.14 | 56 | 3 | 3 | 3.61 |
| | | **Jumla Ndogo** | **987** | **569.68** | **189** | **108** | **8** | **0.81** |
| | | | | | | | | |
| 22 | Simiyu | Busega District Council | 98 | 116.11 | 0 | 33 | 0 | 0 |
| | | Bariadi District Council | 143 | 93.91 | 34 | 34 | 53 | 37.06 |
| | | Bariadi Town Council | 107 | 61.32 | 34 | 34 | 0 | 0 |
| | | Itilima District Council | 59 | 52.64 | | 2 | 0 | 0 |
| | | Maswa District Council | 76 | 51.11 | 22 | 22 | 0 | 0 |
| | | Meatu District Council | 180 | 8.04 | 4 | 10 | 0 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **663** | **375.09** | **94** | **135** | **53** | **7.99** |
| | | | | | | | | |
| 23 | Singida | Manyoni District Council | 223 | 86.03 | 20 | 28 | 5 | 2.24 |
| | | Ikungi District Council | 92 | 31.20 | 21 | 5 | 0 | 0 |
| | | Iramba District Council | 46 | 35.34 | 8 | 32 | 2 | 4.35 |
| | | Itigi District Council | 87 | 49.55 | 30 | 12 | 16 | 18.39 |
| | | Mkalama District Council | 30 | 12.51 | 23 | 0 | 14 | 46.67 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Singida District Council | 48 | 53.24 | 3 | 5 | 8 | 16.67 |
| | | Singida Municipal Council | 488 | 176.81 | 250 | 41 | 10 | 2.05 |
| | | **Jumla Ndogo** | **1014** | **444.68** | **333** | **123** | **55** | **5.42** |
| | | | | | | | | |
| 24 | Songwe | Mbozi District Council | 136 | 92.17 | 32 | 29 | 3 | 2.21 |
| | | Momba District Council | 64 | 99.40 | 12 | 5 | 0 | 0 |
| | | Ileje District Council | 40 | 19.76 | 38 | 39 | 1 | 2.5 |
| | | Songwe District Council | 25 | 13.54 | 27 | 19 | - | 0 |
| | | Tunduma Town Council | 184 | 113.15 | 58 | 40 | 11 | 5.98 |
| | | **Jumla Ndogo** | **449** | **338.02** | **167** | **132** | **15** | **3.34** |
| | | | | | | | | |
| 25 | Tabora | Kaliua District Council | 90 | 39.50 | 3 | 9 | 0 | 0 |
| | | Igunga District Council | 144 | 91.08 | 0 | 11 | 9 | 6.25 |
| | | Urambo District Council | 88 | 64.71 | 38 | 82 | 8 | 9.09 |
| | | Nzega District Council | 278 | 298.01 | 0 | 7 | 4 | 1.44 |
| | | Nzega Town Council | 151 | 34.42 | 37 | 37 | 6 | 3.97 |
| | | Sikonge District Council | 69 | 4.2 | 0 | 24 | 0 | 0 |
| | | Uyui District Council | 53 | 26.75 | 6 | 6 | 0 | 0 |
| | | Tabora Municipal Council | 383 | 194.86 | 0 | 188 | 12 | 3.13 |
| | | **Jumla Ndogo** | **1105** | **714.91** | 84 | **364** | **39** | **3.53** |
| | | | | | | | | |
| 26 | Tanga | Muheza District Council | 236 | 219.15 | 0 | 24 | 0 | 0 |
| | | Handeni District Council | 76 | 39.88 | 16 | 16 | 0 | 0 |
| | | Handeni Town Council | 85 | 57.89 | 10 | 9 | 1 | 1.18 |
| | | Korogwe District Council | 86 | 51.42 | 4 | 13 | 0 | 0 |
| | | Korogwe Town Council | 163 | 33.92 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | Bumbuli District Council | 11 | 6.41 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| | | Lushoto District Council | 71 | 51.52 | 0 | 12 | 0 | 0 |
| | | Mkinga District Council | 201 | 138.52 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | Pangani District Council | 314 | 395.32 | 0 | 17 | 0 | 0 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kilindi District Council | 64 | 56.71 | 0 | 7 | 0 | 0 |
| | | Tanga City Council | 786 | 386.46 | 497 | 291 | 0 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **2093** | **1437.20** | **527** | **393** | **1** | **0.05** |
| | | **JUMLA KUU** | **34,689** | **24,487.19** | **8980** | **10237** | **1,709** | **4.93** |
| | | | | | | | | |
| | | **MUHTASARI** | | | | | | |
| | | IDADI YA MAENEO | **34,689** | | | | | |
| | | YALIYOVAMIWA | **1,709** | | | | | |
| | | UKUBWA WA MAENEO (Hekta) | **24,487.19** | | | | | |

*Chanzo: Mamlaka za upangaji, Septemba, 2024*